

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

KUSITISHWA KWA MUDA KWA USAJILI, UINGIZAJI NA MATUMIZI YA MAZIWA AINA YA LACTOGEN 1 NA NIDO 1 KUTOKA AFRIKA KUSINI

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), imesitisha kwa muda usajili na uingizaji nchini wa maziwa ya watoto aina ya **Lactogen 1 na NIDO 1 kutoka Afrika Kusini** mpaka hapo itakapotangazwa vinginevyo. Uamuzi huu unatokana na taarifa kutoka jimbo la Kwazulu Natal Afrika ya Kusini zinazoeleza kuwepo kwa tatizo la uchafuzi wa maziwa ya **Lactogen 1 toleo Na. 82050179L1 la tarehe 23 Julai 2008 na NIDO 1 toleo Na. 81790181S02E1M la tarehe 27 Juni 2008** nchini Afrika Kusini uliotokana na kemikali iitwayo *melamine*.

Imethibitika kuwa ikiwa mtoto atakula maziwa yenye kemikali ya *melamine* anaweza kupata madhara ya kuharibika kwa figo. Dalili za madhara hayo ni pamoja na mtoto kupata mkojo mara chache kuliko kawaida, kulia wakati wa kukojoa, kutopata mkojo kabisa au kutoa mkojo wenye uchafu. Dalili nyingine ni mtoto kupata shinikizo la damu na endapo kutakuwa na mgandamizo wa eneo la figo basi atapata maumivu makali.

Awali iliripotiwa kuwa, huko nchini China hadi kufikia tarehe 18/09/2008 idadi ya watoto 6244 wenye umri chini ya mwaka mmoja waliugua kutokana na kunywa maziwa yenye kemikali aina ya Melamine, ambapo kati ya watoto hao, wanne walipoteza maisha.

TFDA inapenda kuwatangazia wananchi kuwa kufuatia tishio hilo imechukua hatua za kuhakikisha kuwa maziwa aina ya **Lactogen 1 toleo Na. 82050179L1 la tarehe 23 Julai 2008 na NIDO 1 toleo Na. 81790181S02E1M la tarehe 27 Juni 2008 kutoka Afrika Kusini** hayaingizwi nchini Tanzania kwa lengo la

kulinda afya ya wananchi. Aidha utaratibu unaendelea kufanyika kuhakikisha kuwa bidhaa zote za matoleo hayo (batch) kutoka Afrika ya Kusini haziingii nchini na zilizokwisha ingia katika soko la Tanzania haziwafikii walaji. Hivyo basi TFDA kupitia wakaguzi wa Ofisi za TFDA za Kanda, Vituo vya mipakani na Halmashauri imeelekeza kufanyika ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya nchi ili ikiwa watabaini maziwa ya **Lactogen 1 toleo Na. 82050179L1 la tarehe 23 Julai 2008 na NIDO 1 toleo Na. 81790181S02E1M la tarehe 27 Juni 2008 kutoka Afrika Kusini** wayaondoe sokoni mara moja.

TFDA inawashauri wananchi kuacha kununua maziwa na ambayo hayana lebo au yenye lebo zinazotiliwa mashaka. Pia kusitisha matumizi ya maziwa ya watoto aina ya **Lactogen 1 na NIDO 1 kutoka Afrika Kusini** mpaka hapo watakapopewa maelekezo mengine.

Wafanyabiashara wenye bidhaa husika wanatakiwa wasitishe kuziuzua kwa walaji na watoe taarifa kwenye Ofisi za TFDA au ofisi za Afya zilizo karibu nao. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa watakapo kaidi agizo hili.

Vilevile TFDA inatoa wito kwa wananchi iwapo watagundua kuwepo kwa bidhaa za maziwa ya **Lactogen 1 toleo Na. 82050179L1 la tarehe 23 Julai 2008 na NIDO 1 toleo Na. 81790181S02E1M la tarehe 27 Juni 2008 kutoka Afrika Kusini** watoe taarifa katika Ofisi ya Afya ya Wilaya au Mkoa, Ofisi za Kanda za TFDA zilizopo Mwanza, Arusha na Mbeya au Ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa Makao Makuu zilizopo eneo la External – Mabibo, Dar es Salaam kwa ajili ya ufuatiliaji

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Chakula na Dawa
S.L.P 77150
Dar es salaam

Simu na. 255 22 2450512, 2452108
0787 555 527, 0754 772 220
Fax Na. 255 22 2450793
Barua Pepe : info@tfda.or.tz
Tovuti: www.tfda.or.tz